




Biro ya Grefyé



Picha: ICC-CPI

Biro ya Grefyé ni moya mu bitu ine byenye binaunda Mahakama ya Kimataifa ya Jinai. Inaangaliaka maneno ya uongozi na ya huduma za Mahakama yenye haiko ya kimahakama. Kazi zote za Biro ya Grefyé ziko na nia wazi ya kusaidia Mahakama kutimiza mipango yake.

Kanuni ya kutokuwa na upendeleo mu hali yoyote njo inatawala kazi za Biro ya Grefyé. Biro ya Grefyé inajua matokeo yenye buzuri, ufanisi, uwazi na kuheshimia wakati mu kazi zake binaweza kuwa nayo ku mipango yote ya Mahakama. Ile biro inatumia mkataba na sheria za kimataifa na imeendelea mbele, sana sana mu maneno ya teknolojia za habari na maongezi.

Kutimiza sheria muzuri

Kazi ya lazima ya Biro ya Grefyé ni kufanya kwa ginsi masambo mbele ya batu bote, ya haki, ya muzuri na ya mbiyo ifanyike.

Idara ya waathiriwa na mawakili yenye iko mu Biro ya Grefyé inasaidiaka benye banawaziwa kama balifanya enfraksyo na benye kushtakiwa kusimamiwa na avoka wa Utetezi na, kufuatana na kanuni ya usawa wa haki mbele ya Mahakama, inasaidiaka baavoka ba Utetezi kufanya mapashwa yabo. Tena inasaidiaka baviktime mu byenye binaangalia ginsi banaweza kuwa na neno mu masambo na ginsi banaweza kuomba malipo mbali mbali.

Idara ya huduma za Mahakama inasaidiaka mu maankete na masambo wakati inafanya kazi za lazima sawa vile kuchunga batemwé na kuongoza munyoro ya Mahakama. Tena inafanyaka kazi za kutafsiri makartsi wala maneno mu mikusanyo yote ya masambo na ayo njo inawekaka madosyé, inatiaka mu dosyé makartasi na bitu banaleta, inapashaka habari mbali mbali na inashurulikaka na uongozi ya kimahakama.

Kazi za Tawi la habari na hifadhi ya hati zinasaidiaka kutimiza sheria muzuri ju ile tawi inafanyaka nguvu kusudi masambo ifanyike mbele ya batu bote na bote baweze kuifuata, sana sana batu ba mubikundi byenye bililumizwa na maenfraksyo za kabambi zenye Mahakama iko na uwezo ya kufuatilia.

Ku ngambo yake, Tawi la ulinzi na usalama inasaidiaka kusudi maankete na masambo bipitike muzuri ju inachungaka usalama ya bote benye kusamba.

Taasisi yenye inaitikiwa na yenye iko na msaada yenye inafaa

Biro ya Grefyé inaongeaka mara mingi na bikundi mingi byenye binajishurulisha na kazi za Mahakama, mu bitu sawa vile habari, kufundisha batu na uhusiano na inje. Kazi za uhusiano na inje ziko na nia ya kufanya kwa ginsi kupatikane msaada ya mainchi na bikundi bya mainchi mu kazi sawa zile za kuchunga batemwé, za kutimiza malipizi yenye Mahakama ilipana, za kubadilishana habari, za kupata na kubeba bitu bya lazima fasi ya kazi na za usalama. Bikundi byenye habiko bya leta, benye banatumika kazi za sheria, na batumishi ba mainiversité bako na mafaa sana mu mfumo ya sheria ya kimataifa yenye kuangaliana na maenfraksyo. Biro ya Grefyé iko ndani ya ile mfumo. Ni Biro ya karibu sana ya Grefyé njo iko kabisa na kazi ya kuanza na kuendelea maongezi na bikundi byenye binajishurulisha na kazi za Mahakama.

Tawi la maoni ya kisheria na Tawi la habari na hifadhi ya hati nazo ziko na mafaa mu ile uhusiano na bikundi byenye binajishurulisha na kazi za Mahakama. Tena, matawi zingine, sawa vile Tawi la ushirikishwaji wa waathiriwa na la malipo, Kitengo cha msaada kwa waathiriwa na mashahidi na tena Tawi la zuizi, haziwezi kufanya mapashwa yake muzuri bila kuwa na maongezi

mara mingi na bile bikundi byenye habiko bya Mahakama. Kazi ya kufundisha batu ni ya lazima sana juu ya kutimiza nia ya Mahakama : kuwa taasisi yenye inaitikiwa na yenye inaungwa mkono. Biro ya Grefyé iko na kazi ya kufanya na kutayarisha mupango ya habari na ya kufundisha batu kufuatana na mupango wa mkakati wa Mahakama yenye kuangaliana na ile kazi. Mahakama inapashwa kufanya juhudi juu ikuwe karibu ya bikundi ya batu benye balipatikana na misiba. Njo mana inapashwa kufanya namuna muzuri ya uhusiano mu njia mbili kusudi ijuwe muzuri shida za bale batu na byenye banatumainia na ivi iweze kubasaidia kusadiki sana mfumo wa kisheria wa kimataifa.

Mfano ya utawala

Matawi mbali mbali, sawa vile Ofisi ya mdhibiti, Tawi la utumishi, Tawi la bajeti na usimamizi wa fedha wala Tawi la ulinzi na usalama na tena Tawi la maoni ya kisheria,

zote zinafanyaka kazi ya lazima wakati zinapangaka namuna muzuri ya utawala yenye hailete buzito ku Mahakama.

Idara ya huduma za utawala kwa wote inafanyaka kazi za teknolojia ya habari, mupango ya muzuri ya bajeti, hesabu ya kweli ya franka, inapokeaka mali na kupanga ginsi ya kupata na kugawa bitu, inafanyaka nguvu kusudi mabiro za inje za Mahakama zitumike muzuri na kushurulikia hali muzuri ya manyumba za Mahakama. Hizi kazi zote na zingine zinasaidiaka Mahakama kuwa taasisi ya mafaa, nyepesi tena yenye inaangaikia mapashwa yake.

Ni mu ile juhudi njo Tawi la utumishi inafanyaka kazi ya mafaa wakati inasemaka na kutimiza nia zenye zinapatana na kitu cha maana sana chenye Mahakama iko nacho : batumishi bake.



© ICC-CPI/Max Koot

Ju ya Grefyé

Biro ya Grefyé inasimamiwa na Grefyé, yeye njo mkubwa mwenye anaangalia maneno ya uongozi ku Mahakama na alichaguliwaka kwa siri na wingi kabisa ya bajije benye balikuwaka mu mukusanyo ya bote. Bi. Silvana Arbia kutoka Italie alichaguliwaka, siku 28 ya mwezi ya pili, kuwa Grefyé wa mupya muda ya miaka tano. Amekamata fasi kwenye Bw. Bruno Cathala anatoka. Bi. Arbia atakuwa chini ya mamlaka ya Prezida wa Mahakama.

Bi. Arbia anazoweya sana sheria ya kimataifa, sheria yenye kuangaliana na maenfraksyo na tena sheria ya kimataifa yenye kuangaliana na maenfraksyo, sana sana mu byenye binaelekea ginsi ya kuongoza kazi za mahakama. Mbele aanze kutumika ku Mahakama ya Kimataifa ya Jinai alikuwaka mkubwa mwenye anasimamia mashtaka ku Mahakama ya Kimataifa ya Jinai ya Rwanda (ICTR) kisha kuwa *Senior Trial Attorney* na mkubwa wa mshtaka kwa muda mu Biro ya Prokirere na hivi akasimamia mashtaka mu afere za kabambi mbele ya ile Mahakama. Tena, wakati ya mkutano ya mabalozi ya 1998 pale Roma, Bi. Arbia, sawa vile moya mu benye balitumiwaka na Italie, alitumikaka ku kazi za kutayarisha Mkataba wa Roma wa Mahakama ya Kimataifa ya Jinai. Bi. Arbia iko na cheti ya *Laurea* mu sheria yenye alipataka ku iniversité ya Padova kule Italie na alikuwaka jije Italie. Aliandikaka makartasi na bitabu mingi juu ya haki za binadamu na za batoto.

